# UWEZO WA WAUGUZI KUZUIA MTU ANAYETIBIWA KWA SHIDA YA AKILI KAMA MGONJWA ALIYELAZWA HOSPITALI

(Sehemu ya 5(4) ya Sheria ya Afya ya Akili 1983)

| | |
|---|---|
| 1. Jina la Mgonjwa | |
| 2. Jina la mtu anayesimamia matibabu yako | |
| 3. Jina la mtu anayesimamia matibabu yako | |

## Je! ni kwanini siwezi kutoka katika hospitali hii?

Unawekwa hospitalini chini ya sehemu ya 5(4) ya Sheria ya Afya 1983. Hii ni nguvu halali inayomruhusu muuguzi kukuweka hospitalini hadi ukishaonwa na mtu anayesimamia matibabu yako, au msaidizi wake. Muuguzi anaamini unayo shida ya akili na hauruhusiwi kutoka.

“Msaidizi” inamaanisha mtu anayeweza kufanya uamuzi wakati mtu anayesimamia matibabu yako yuko mahali pengine.

## Je! nitawekwa hapa kwa muda gani?

Lazima ukae katika hospitali hii kwa muda wa hadi masaa sita hadi mtu anayesimamia matibabu yako au masaidizi wake aseme unaweza kuenda. Ukijaribu kutoka, wafanyikazi wanaweza kukuzuia, na ikiwa utatoka, unaweza kurudishwa.

Katik akesi yako masaa sita yanaisha:

| Tarehe | Saa |
|---|---|
| | |

Ikiwa mtu anayesimamia matibabu yako au msaidizi wake hajakuona kufikia wakati huu, utakuwa huru kuenda. Lakini ukiamua kuenda basi, tafadhali uliza muuguzi au mfanyikazi kwanza.

